# JINSI COVID-19 INAVYOHUSIANA NA HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU: MWONGOZO


1. Je, COVID-19 imeathiri vipi haki ya kupokea huduma za afya kwa watu wenye ulemavu?
2. Je, COVID-19 imewaathiri vipi watu wenye ulemavu wanaoishi katika taasisi mbalimbali?
3. Je, COVID-19 imeathiri vipi watu wenye ulemavu kuishi katika jamii?
4. Je, COVID-19 imeathiri vipi ajira, mapato na riziki ya watu wenye ulemavu?
5. Je, COVID-19 imeathiri vipi haki ya kupata elimu kwa watu wenye ulemavu?
6. Je, COVID-19 imeathiri vipi haki ya kulindwa dhidi ya dhuluma kwa watu wenye ulemavu?
7. Je, COVID-19 imeathiri vipi makundi mahsusi ya watu yanayojumuisha kwa kiasi kikubwa watu wenye ulemavu?
    a. wafungwa wenye ulemavu
    b. watu wenye ulemavu wasio na makao yanayofaa


## MUHTASARI


Ingawa janga la  COVID-19 limeathiri wanajamii wote, watu wenye ulemavu wameathirika zaidi kutokana na vikwazo vya kimtazamo, kimazingira na kitaasisi ambavyo bado vinawakabili katika mchakato mzima wa kupambana na COVID-19.

Watu wengi wenye ulemavu pia wana matatizo mengine ya kiafya yanayowafanya wawe katika hatari zaidi ya kuambukizwa virusi hivi, kupata dalili kali zaidi wanapoambukizwa hivyo kusababisha ongezeko la idadi ya vifo. Wakati wa janga la COVID-19, watu wenye ulemavu wanaotegemea familia zao wanaweza kujipata wametengwa na huenda wasiweze kuendesha maisha yao wakati wa kutekelezwa kwa kanuni za kudhibiti shughuli za kawaida, huku wanaoishi katika taasisi mbalimbali wakiathirika, kama inavyobainika kutokana na idadi kubwa ya vifo katika makaazi ya utunzaji na hospitali za wenye akili punguani. Vikwazo katika kupata maelezo na huduma za afya kwa watu wenye ulemavu vimezidi kukithiri. Watu wenye ulemavu pia wanazidi kukabiliwa na ubaguzi na vikwazo vingine katika kujikimu kimaisha na kupokea mapato, kushiriki katika masomo ya mtandaoni na kulindwa dhidi ya dhuluma. Makundi mahsusi ya watu wenye ulemavu , kama vile wafungwa na wasio na makao au makaazi yanayofaa wanakabiliwa na hatari kubwa zaidi.

Kufahamu kuwa hatari hizi zipo kunasaidia masuala haya kushughulikiwa kwa njia bora zaidi ili kuwalinda watu wenye ulemavu wasiathirike. Madhumuni ya mwongozo huu ni:

- kuhamasisha kuhusu athari za janga kwa watu wenye ulemavu  pamoja na haki zao;
- kuangazia mipango mwafaka inayotekezwa kote ulimwenguni;
- kubaini hatua muhimu kwa Nchi na washikadau wengine; na
- kutoa nyenzo za kuelimisha zaidi kuhusu kukabiliana na COVID-19 kwa njia inayolinda haki za kibinadamu zikiwemo haki za watu wenye ulemavu.


## 1. JE, COVID-19 IMEATHIRI VIPI HAKI YA KUPOKEA HUDUMA ZA AFYA KWA WATU WENYE ULEMAVU?

Licha ya kuwa watu wenye ulemavu wako katika hatari ya kuambukizwa COVID-19, wanakabiliwa na changamoto hata zaidi katika kupokea huduma za kimatibabu wakati wa janga hili kutokana na vizingiti vya kufikia maelezo na vituo vya afya, pamoja na kutozingatiwa katika masharti na kanuni za afya zilizowekwa. Hivyo, hali hii inawabagua zaidi watu wenye ulemavu katika kupokea huduma za afya. Wakati mwingine, kanuni hizi huonyesha ubaguzi wa kupokea matibabu kwa watu wenye ulemavu kulingana na hadhi na nafasi yao katika jamii. Kwa mfano, kanuni za utaratibu wa kutoa tiba adimu kwa wagonjwa mahsusi pekee kulingana na aina fulani za ulemavu, mgonjwa kuwa mwenye utegemezi sana, "udhaifu", uwezekano wa "kufaulu kwa matibabu", pamoja na ukadiriaji wa "miaka ya kuishi" iliyosalia endapo mgonjwa atapona. Watu wenye ulemavu pamoja na familia zao pia wanashinikizwa na watoa huduma wa afya kupuuza masharti ya kimatibabu ya kumrudishia mgonjwa fahamu.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

- Kamati ya Maadili ya Kimatibabu ya **Jamhuri ya San Marino** imeweka mwongozo wa COVID-19 kuhusu utaratibu wa kutoa matibabu, unaopiga marufuku ubaguzi kwa misingi ya ulemavu: "Hivyo, kigezo kinachopaswa kutumika pekee, ni kuzingatia utaratibu unaofaa wa kupokea matibabu, kwa kulinda maisha ya kila mtu, kulingana na hali ya afya na kiwango cha matibabu. Kimaadili, vigezo vingine kama vile umri, jinsia, jamii au kabila na ulemavu havifai kutumika kwani vinaleta dhana kuwa maisha ya watu fulani ni muhimu zaidi kuliko wengine. Huu ni ukiukaji wa haki za kibinadamu."[1]
- Ofisi ya Haki za Raia kwenye Idara ya Huduma za Afya na Jamii nchini **Marekani** imetoa tangazo ili kuhakikisha kuwa mamlaka mbalimbali zinapiga marufuku ubaguzi kwa misingi ya ulemavu, wakitaja kuwa "watu wenye ulemavu hawapaswi kunyimwa huduma za kimatibabu kwa misingi ya dhana potovu, tathmini za hali ya maisha yao, au maamuzi kuhusu "hadhi" ya mtu kwa misingi ya umri au ulemavu".[2] Tangazo lenyewe pia linatoa mwongozo kwa mamlaka mbalimbali kuhakikisha watu wenye ulemavu wamehamasishwa na wanaweza kupata maelezo ili pawe na usawa na waweze kunufaika kutokana na juhudi za kutoa huduma za dharura, "ikiwemo kuwapa mahali pa kukaa [ili] kusaidia kuhakikisha kuwa utoaji huduma za dharura umefaulu na kupunguza unyanyapaa."
- **Muungano wa Falme za Kiarabu** umezindua mpango wa kitaifa wa kuwapima watu wenye ulemavu nyumbani kwao na kufikia katikati ya mwezi Aprili, watu 650,000 wenye ulemavu walikuwa wamepimwa COVID-19 .[3]
- Nchini **Ufilipino**, Tume ya Haki za Kibinadamu imechapisha maelezo ya kusaidia mashirika za afya kutoa matangazo ya umma kwa makundi yanayoathirika zaidi katika jamii, wakiwemo watoto na watu wenye ulemavu.[4]
- Nchini **Kanada**, kamati ya Mashauriano kuhusu Athari za COVID-19 kwa Walemavu ilibuniwa kwa kuwashirikisha watu wenye ulemavu pamoja na mashirika yanayowawakilisha ili kufanya mashauriano na serikali kuhusu masuala, changamoto, mahitaji, mikakati, kanuni na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuwashughulikia watu wenye ulemavu.[5]

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- **Kupiga marufuku kunyimwa huduma za matibabu kwa misingi ya ulemavu** na kubadilisha sera zinazomzuia mtu kupokea matibabu kwa misingi ya ulemavu, kiwango cha utegemezi, hali ya maisha au ubaguzi wa kimatibabu wa aina nyingine yoyote dhidi ya watu wenye ulemavu, ikijumuisha ubaguzi kwenye kanuni za utoaji tiba adimu (kama vile mashine za kupumua au kupokea huduma za wagonjwa mahututi).
- **Kipaumbele katika kupimwa** kwa watu wenye ulemavu walio na dalili.
- **Kuhimiza utafiti** kuhusu athari za COVID-19 kwa watu wenye ulemavu.
- **Kutambua na kuondoa vikwazo vya kupokea matibabu** ikiwemo kuhakikisha kuwa wanaweza kufika kwenye vituo vya afya (hospitali, vituo vya upimaji na karantini), pamoja na kuhakikisha maelezo ya afya yanawafikia na yanasambazwa kwa njia na miundo wanayoweza kufikia.
- **Kuhakikisha kuwa madawa yanatolewa na yanawafikia** watu wenye ulemavu wakati wa janga hili**.**

- **Kutoa mafunzo na kuwahamasisha wahudumu wa afya** ili kuzuia ubaguzi kwa misingi ya dhana potovu na upendeleo dhidi watu wenye ulemavu.
- **Kushauriana kwa karibu na watu wenye ulemavu na mashirika yanayowawakilisha** ili kuweka mfumo wa kuwashughulikia wakati wa janga huku haki zao zikilindwa. Mfumo huu ujumuishe watu wote wenye ulemavu tofautitofauti.

**Nyenzo**

- COVID-19 inaathiri watu wote: "Kila mtu ana haki ya kuishi" – wataalam wa Umoja wa Mataifa walisema
- Ripoti ya Mtaalam Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu, COVID-19: Je, ni nani anayewalinda watu wenye ulemavu?
- Shirika la Afya Ulimwenguni, Kuwashughulikia watu wenye ulemavu wakati wa janga la COVID-19

## 2. JE, COVID-19 IMEWAATHIRI VIPI WATU WENYE ULEMAVU WANAOISHI KATIKA TAASISI MBALIMBALI?

COVID-19 imeathiri vikali hospitali za wenye akili punguani, makaazi ya utunzaji (makao ya mayatima, vituo vya utunzaji wa mchana, vituo vya kurekebisha tabia) na makao ya wakongwe, hivyo kupelekea ongezeko la maambukizi na idadi ya vifo. Baadhi ya tafiti za awali zilionyesha kuwa, idadi ya vifo katika makaazi ya utunzaji yalikuwa asilimia 42 hadi 57 ya idadi jumla ya vifo kutokana na COVID-19 katika nchi hizo.[6] Watu wenye ulemavu wanaoishi katika taasisi mbalimbali wako hatarini zaidi katika kuambukizwa COVID-19 kutokana na matatizo mengine ya kiafya, changamoto ya kutangamana kwa ukaribu miongoni mwa wakaaji na wafanyakazi na kutoshughulikiwa na wahudumu. Watu wenye ulemavu wanaoishi katika taasisi mbalimbali pia wako wanakabiliwa na hatari ya ukiukaji wa haki za kibinadamu, kama vile kutoshughulikiwa, kushururishwa, kutengwa na kudhulumiwa.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

- Nchini **Uswizi** na **Uhispania,** watu wenye ulemavu wanaoishi katika taasisi mbalimbali walihamishwa na kupelekwa kwa familia zao, ikiwezekana.
- Nchini **Kanada,** mwongozo kuhusu upimaji uliopewa kipaumbele ulitolewa na unajumuisha kanuni mahsusi za kitaasisi.[7]

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- **Kuwaondoa watu wenye ulemavu kutoka kwenye taasisi** na kuhakikisha kuwa wanapokea usaidizi katika jamii kupitia familia na/au njia zisizo rasmi, na pia kufadhili huduma za usaidizi wanazopokea kutoka kwa watoa huduma wa umma na binafsi.
- **Kwa sasa, upimaji upewe kipaumbele na tahadhari zichukuliwe** katika taasisi ili kupunguza visa vya maambukizi kwa kushughulikia suala la msongamano wa watu, kuhakikisha watu hawakaribiani, kubadilisha saa za wageni kuzuru, kusisitiza utumiaji wa vifaa vya kujilinda na kudumisha usafi.
- **Kuongeza raslimali katika taasisi *kwa muda*** ikijumuisha wafanyakazi na fedha ili kutekeleza tahadhari za kuzuia maambukizi.
- **Wakati wa hali ya dharura, haki za watu wenye ulemavu wanaoishi katika taasisi mbalimbali zizidi kulindwa** ikiwemo haki ya kulindwa dhidi ya ukandamizaji, dhuluma na ubaguzi, haki ya kutoa idhini bila kushurutishwa na haki ya kulindwa na sheria.[8]
- **Kupata afueni kwa kuweka na kutekeleza mikakati ya kuwaondoa hospitalini wenye akilini punguani** kwa kufunga taasisi na kuwarejesha katika jamii, na kuunga mkono huduma za usaidizi kwa watu wenye ulemavu na wakongwe.

**Nyenzo**

- Shirika la Afya Ulimwenguni, mwongozo wa Kuzuia na Kudhibiti Maambukizi kwa Vituo vya Matibabu ya Muda Mrefu wakati wa janga la COVID-19, Mwongozo wa muda, 21 Machi 2020
- Shirika la Afya Ulimwenguni, Kuwashughulikia watu wenye ulemavu wakati wa janga la COVID-19
- Taarifa kutoka kwa mashirika ya kieneo na kimataifa ya watu wenye ulemavu wa kiakili pamoja na mapendekezo kuhusiana na janga la COVID-19

## 3. JE, COVID-19 IMEATHIRI VIPI HAKI YA WATU WENYE ULEMAVU KUISHI KATIKA JAMII?

Watu wenye ulemavu wanakabiliwa na vikwazo kila siku katika jamii kutokana na kanuni zilizowekwa za kukabiliana na COVID-19. Hasa, masharti ya kusalia nyumbani yasiyozingatia mahitaji yao yanawatatiza na yanaathiri uhuru, afya na maisha yao.[9]

Watu wengi wenye ulemavu wanaowategemea wengine katika kuendesha maisha yao (kupitia usaidizi rasmi wa watoa huduma au usio rasmi unaotolewa na jamaa/marafiki) wanajipata bila msaada kutokana na kanuni zilizowekwa za kutokaribiana na kutotoka sehemu moja hadi nyingine. Huenda hali hii ikawaweka katika hatari ya kutopata chakula, madawa, bidhaa muhimu na inaweza kuwazuia kufanya shughuli muhimu za kila siku kama vile kuoga, kupika au kula.

Maelezo ya umma kuhusu kanuni za COVID-19 hayatolewi wala hayasambazwi kupitia miundo na njia zinazowafikia watu wote wenye ulemavu (mf. ufasiri wa lugha ya ishara, uwekaji manukuu, muundo Unaosomeka kwa Rahisi, nk).

Isitoshe, baadhi ya watu wenye ulemavu, kama vile walio na matatizo ya kiakili na wasioweza kuwasiliana vyema, huenda wakaathiriwa na masharti kali ya kusalia nyumbani. Matembezi mafupi yanayofanywa kwa uangalifu kila siku ni muhimu katika kuwawezesha kuzoea hali iliyopo.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

- Nchi za **Paragwai**[10] na **Panama**[11] zimebuni mifumo ili kuhakikisha maelezo muhimu yanatolewa kwa njia zinazoweza kufikiwa na watu wote. Vilevile, Wizara ya Afya ya **Nyuzilandi** imetenga sehemu maalum kwenye tovuti yake ili kutoa maelezo katika miundo inayoweza kutumiwa na watu wote ikiwemo lugha ya ishara na muundo unaosomeka kwa urahisi.[12] Serikali ya **Meksiko** imefuata mkondo huu.[13]
- Nchini **Ajentina,**[14] wanaotoa usaidizi kwa watu wenye ulemavu wanaruhusiwa kutoka sehemu moja hadi nyingine na kutangamana kwa ukaribu ili waweze kuwashughulikia. Mashirika ya usaidizi wa kijamii yameibuka nchini **Kolombia** na yanawajumuisha wafanyakazi wa kujitolea wanaowasaidia watu wenye ulemavu na wakongwe katika kununua vyakula na bidhaa zingine.[15] Pia, nchini **Panama**, katika juhudi za kupunguza hatari, watu wenye ulemavu pamoja na wanaowasaidia wametengewa saa maalum za kunua bidhaa muhimu.[16]
- **Muungano wa Uingereza na Ayalandi Kaskazini**[17] umelegeza masharti kali ya awali ya kujitenga na kuwaruhusu walio na matatizo ya kiakili na watu wengine wenye ulemavu kutoka nje. Nchi ya **Ufaransa** pia imeweka kanuni sawa.[18]

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- Kuhakikisha kuwa **maelezo kuhusu kanuni za COVID-19 yanafikiwa na** watu wenye ulemavu, ikiwemo kupitia ufasiri wa lugha ya ishara, utumiaji manukuu, miundo inayosomeka kwa urahisi na mengineyo.
- Kuhakikisha kuwa **wanaowasaidia watu wenye ulemavu wanaruhusiwa kutoka nyumbani** ili kuwawezesha kutoa huduma za usaidizi.
- Kuhimiza na kuratibu **usitawi wa mipango ya usaidizi wa kijamii**, na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa, nyenzo na vifaa vya kujikinga.

- Kuweka **saa za kufungua kwa kuwapa kipaumbele** watu wenye ulemavu na wale wanaowasaidia katika maduka makuu, ya vyakula na maduka mengine muhimu, wakati wa kutekelezwa kwa amri ya kutotoka nje.
- **Kuhakikisha kanuni zinawajumuisha na kuwalinda** watu wenye ulemavu kwa kuweka sheria inayowaruhusu kutoka nyumbani, kutowatoza faini na kuwaruhusu kutoka nje.

**Nyenzo**

- Shirika la Afya Ulimwenguni, Kuwashughulikia watu wenye ulemavu wakati wa janga la COVID-19
- UNPRPD, ILO na mashirika mengine, Ulinzi wa kijamii kwa walemavu wakati wa janga la covid-19

## 4. JE, COVID-19 IMEATHIRI VIPI AJIRA, MAPATO NA RIZIKI YA WATU WENYE ULEMAVU?

Uwezekano wa watu wenye ulemavu kuajiriwa uko chini ikilinganishwa na watu wengine, na hata wanapoajiriwa, uwezekano ni kuwa wao huishia katika ajira isiyo rasmi.[19] Hivyo, kulingana na ajira, bima yao ya jamii iko chini ikilinganishwa na wengine na hili linaathiri uwezo wao wa kujikimu wakati wa huu wa janga la COVID-19. Kwa walioajiriwa au waliojiajiri,[20] huenda wasiweze kufanyia kazi nyumbani kutokana ukosefu wa zana za kazi na usaidizi unaotolewa kazini, na hivyo wanakabiliwa na hatari ya kupoteza mapato na ajira. Isitoshe, kanuni za COVID-19 huenda zinawaathiri watu wenye ulemavu vinginevyo kwa kuzuia wanafamilia na wanaokimu mahitaji ya familia kwenda kazini, hivyo kuathiri mapato ya familia kwa jumla. Ukosefu wa mapato ni mzigo kwa watu wenye ulemavu pamoja na familia zao ambazo kawaida hugharamikia malipo mengine ya ziada yanaohusiana na ulemavu (makaazi za zana zinazohitajika, vifaa saidizi, huduma na bidhaa maalum, nk), na hali hii huwapelekea kuishia kuwa maskini.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

- Katika kukabiliana na COVID-19, nchi za **Bulgaria, Malta** na **Lithuania** zimeongeza mgao wa fedha unaotolewa kwa huduma za ulinzi wa jamii ili kupanua huduma za usaidizi za kijamii na kuwajumuisha watu zaidi, wakiwemo watu wenye ulemavu.[21]
- Nchini **Ajentina** na **Peru**, watu wanaonufaika kutokana na mpango wa kuwasaidia walemavu watapokea nyongeza ya kiasi wanachopokea ili kuwawezesha kukabiliana na COVID-19.[22] Nchi ya **Ufaransa** imetangaza mkakati sawa utakaowafaidi wanaopokea pesa kutokana na ulemavu,[23] nayo nchi ya **Tunisia** imeweka mpango wa dharura unaojumuisha kutoa pesa kwa wenye mapato ya chini, watu wenye ulemavu na wasio na makao.[24]
- Nchi ya **Marekani**[25] imeweka mipango ya ondoleo la ushuru hivyo kusaidia kupunguza mzigo wa kifedha kwa watu wenye ulemavu wakati huu wa janga.

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- Kutoa **usaidizi wa kifedha kwa watu wenye ulemavu wasio na mapato yoyote** (mf. kuwapa mkupuo; kuwaondolea ushuru, kuwapunguzia bei za bidhaa, nk.).
- **Kuongeza manufaa wanayopokea watu wenye ulemavu**, ikijumuisha kutoa malipo mapema ili kushughulikia gharama za ziada.
- **Kuongeza kiotomatiki** muda wa kukamilisha malipo yanayohusiana na ulemavu ikiwa tarehe ya kulipa imekaribia.
- Kutoa **fidia ya kifedha** kwa watu wenye ulemavu walioajiriwa na mapato yao kupunguzwa.
- Kutekeleza **mipango ya usaidizi wa kifedha** kwa watu walioacha kazi ili kuwasaidia au kuwakinga wanafamilia wenye ulemavu dhidi ya kuambukizwa, na wasio na bima ya afya au inayowafidia hata ikiwa hawako kazini.
- Kutoa **usaidizi wa kifedha, ikiwemo kupitia punguzo la ushuru, kwa waajiri** wa wafanyakazi wenye ulemavu ili kugharamikia vifaa wanavyohitaji vya kufanyia kazi nyumbani.
- Kuhakikisha kuwa **mipango ya utoaji chakula inajumuisha** watu wenye ulemavu na inashughulikia mahitaji yao, ikiwemo kuwasafirishia chakula hadi makwao.

**Nyenzo**

- ILO, Hakuna atakayeachwa nyuma, wakati huu, wala kamwe Kuwashughulikia watu wenye ulemavu katika kukabiliana na COVID-19
- UNPRPD, ILO na mashirika mengine, Ulinzi wa Kijamii kwa walemavu wakati wa janga la COVID-19
- Shirika la Fedha la Kimataifa, Sera za kukabiliana na COVID-19

## 5. JE, COVID-19 IMEATHIRI VIPI HAKI YA KUPATA ELIMU KWA WATU WENYE ULEMAVU?

Uwezekano wa watu wenye ulemavu kukamilisha masomo uko chini ikilinganishwa na watu wengine, na huenda wakakosa kujumuishwa katika masomo kabisa.[26] Kutokana na COVID-19, Nchi nyingi zimefunga taasisi za elimu kwa muda[27] hivyo wanafunzi wote wameathirika wakiwemo wanafunzi wenye ulemavu. Ili kupunguza athari za kukatizwa kwa shughuli za masomo, baadhi ya Nchi zinatumia mfumo wa masomo ya mtandaoni. Hata hivyo, katika hali hii, wanafunzi wenye ulemavu wanakabiliwa na vikwazo kutokana na changamoto za kutokuwa na vifaa vinavyohitajika, kukosa muunganisho wa intaneti, nyenzo na usaidizi wanaohitaji ili waweze kushiriki katika masomo yanayotolewa na shule zao mtandaoni. Kwa sababu hiyo, wanafunzi wengi wenye ulemavu wameachwa nyuma kimasomo, hasa wanafunzi wenye ulemavu wa kiakili.

Zaidi ya hayo, wanafunzi wenye ulemavu pia wameathirika vinginevyo kutokana na kufungwa kwa shule, ikiwemo kukosa chakula inayotolewa shuleni na kunyimwa fursa ya kushiriki na wenzao katika michezo.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

- Nchi ya **Marekani** imetoa hati ya mwongozo kuhusu sheria husika za serikali, Sheria Inayowalinda Watu wenye Ulemavu.[28]
- Nchi ya **Ekwado** imetoa mapendekezo kwa waalimu kuhusu kutoa usaidizi wa kielimu kwa watoto waliotengwa nyumbani.[29]
- **Muungano wa Uingereza na Ayalandi Kaskazini** umetoa maelezo na kuweka mifumo ya kuwasaidia wazazi na watunzaji kufahamu jinsi ya kutekeleza majukumu anuwai nyumbani na vilevile kuwasaidia watoto wenye ulemavu kupata elimu.[30]

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- **Kutoa mwongozo wa kina** kwa mamlaka za elimu na shule kuhusu majukumu yao na nyenzo zinazopatikana wakati wa utoaji wa masomo nje ya muktadha wa shule.
- **Kuhakikisha kuna muunganisho wa Intaneti kwa masomo ya mtandaoni na kuhakikisha kuwa programu zinaweza kutumiwa** na watu wenye ulemavu, ikiwemo kutoa vifaa saidizi na makao yanayowafaa.
- **Kutoa mwongozo, mafunzo na usaidizi kwa waalimu** kuhusu elimu jumuishi kupitia masomo ya mtandaoni.
- **Kushirikiana kwa karibu** na wazazi na watunzaji katika elimu ya mapema ya watoto wenye ulemavu.
- **Kutoa mwongozo na usaidizi wa mtandaoni kwa wazazi na watunzaji** kuwawezesha kuweka mipangilio ya vifaa na kusaidia mpango wa elimu wa watoto wao wenye ulemavu.
- **Kuandaa nyenzo mahsusi na zinazoweza kutumiwa** na wanafunzi wenye ulemavu, ili kusaidia masomo ya mtandaoni.
- **Kuandaa nyenzo za elimu zinazotumia picha na sauti** ili kutoa mafunzo kupitia njia mbalimbali (k.m. zinazopatikana mtandaoni, vipindi vya kuelimisha, nk.)

**Nyenzo**

- Taarifa ya Kamati ya CRC kuhusu athari hasi za kimwili, kihisia na kisaikolojia kwa watoto kutokana na janga la COVID-19, na mwito kwa mataifa kulinda haki za watoto
- UNICEF, Kukabiliana na COVID-19: Kuwashughulikia Watoto na Watu Wazima wenye Ulemavu
- UNESCO, Tovuti kuhusu Kukabiliana na COVID-19

## 6. JE, COVID-19 IMEATHIRI VIPI HAKI YA KULINDWA DHIDI YA DHULUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU?

Watu wenye ulemavu wako katika hatari kubwa ya kudhulumiwa, hasa wakiwa peke yao. Wanawake na wasichana wenye ulemavu wamo katika hatari zaidi ya ukatili wa kijinsia, kudhulumiwa kimapenzi, kingono na vurugu za kinyumbani.[31] Licha ya kuwa wanawake na wasichana wenye ulemavu wamo hatarini zaidi katika kudhulumiwa ikilinganishwa na wanawake wengine, pia wanadhulumiwa zaidi ya wanaume wenye ulemavu.[32] Ingawa maelezo kuhusu ulemavu na dhuluma za kijinsia kuhusiana na COVID-19 hayapatikani kwa sasa, ni bayana kuwa katika hali kama hii, watu wenye ulemavu wamo hatarini.[33]

Kuripoti, na kupata huduma na usaidizi kuhusu dhuluma za kinyumbani ni changamoto kwa watu wenye ulemavu, kwani huduma hizi kawada hazijumuishi na hazifikiwi na watu wenye ulemavu. Huduma za usaidizi kupitia njia ya simu kawaida hazijumuishi utafsiri kwa wenye matatizo ya kusikia, na wasioona wala kusikia, nayo makaazi na huduma za dharura hazijafikia viwango vya kutimiza mahitaji ya watu wenye ulemavu.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

Nchini **Peru**, mwongozo ulitolewa kwa serikali za mitaa kuwasiliana na watu wenye ulemavu kupitia simu, wakati wa janga, na kuwatembelea baada ya hali ya dharura, kisha waripoti kwa mamlaka husika kuhusu hali ilivyo.[34] Kando na haya, OHCHR haikuweza kubuni mipango mwafaka katika eneo hili. Hali hii inazua wasiwasi. Baadhi ya nchi zinazidi kutoa huduma za usaidizi kupitia simu, usaidizi na kuripoti ikiwemo kupitia SMS, huduma za utafsiri na simu za video kwa wenye watatizo ya kusikia.[35] Nyenzo zilizoorodheshwa hapa chini zinataja baadhi ya mipango mwafaka.

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- **Kuhakikisha kuwa huduma za kupiga ripoti, huduma za usaidizi kupitia simu, makaazi ya dharura na aina zingine za usaidizi zinawajumuisha na zinaweza kufikiwa na watu wenye ulemavu**.
- **Kufuatilia** hali ya watu wenye ulemavu, hasa wanaoishi peke yao, kwa kuhimiza kuwajulia hali mara kwa mara kupitia jamii na mipango ya kujitolea kwa hiari.
- **Kuhamasisha na kutoa mafunzo** kuhusu hatari ya kudhulumiwa inayowakabili watu wenye ulemavu, hasa wanawake na wasichana, na pia kukuza mipango ya usaidizi ikiwemo kuchochea usaidizi wa wanarika.

**Nyenzo**

- UNFPA, Mwongozo kuhusu Utoaji wa Huduma kwa Njia Inayolinda Haki na Kuzingatia Jinsia ili Kushughulikia Dhuluma za Kijinsia na Kulindwa kwa Haki za Uzazi na Kijinsia kwa Wanawake na Vijana wenye Ulemavu
- Huduma Muhimu kwa Waathiriwa wenye Ulemavu Wakati wa Janga la COVID-19

## 7. JE, COVID-19 IMEATHIRI VIPI MAKUNDI MAHSUSI YA WATU YANAYOJUMUISHA KWA KIASI KIKUBWA WATU WENYE ULEMAVU: WAFUNGWA WENYE ULEMAVU NA WALE WASIO NA MAKAO YANAYOFAA.

### a. WAFUNGWA WENYE ULEMAVU

Watu wenye ulemavu ni wengi miongoni mwa wafungwa,[36] hasa wenye ulemavu wa kiakili na walio punguani. Wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa kutokana na msongamano wa watu na mazingira yasiyo safi ambapo watu wanatangamana

kwa ukaribu. Hasa, wafungwa wengi wenye ulemavu wanawategemea wenzao katika kupata chakula, kutembea na kuoga, na kawaida, huduma za afya za magereza hazikithi mahitaji yao.

Changamoto hizi zinawakabili sio tu watu wenye ulemavu walio jela na rumande kupitia mifumo ya mahakama na magereza, bali pia wale waliozuiliwa na mamlaka mbalimbali au kwa njia nyingine, wakiwemo wahamiaji wenye ulemavu waliozuiliwa katika rumande za uhamiaji.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

- Katika **Muungano wa Uingereza na Ayalandi Kaskazini,** wafungwa waliosalia na chini ya miezi miwili kutumikia kifungo wanaachiliwa.[37] Nchini **Marekani**, Jimbo kadhaa zimewaachilia au ziko katika hatua ya kuwaachilia wafungwa.[38] Vilevile, wafungwa pia wameachiliwa nchini **Irani**, **Uturuki** na **Indonesia**. Nchini **Kolombia**, watu wenye ulemavu waliowekewa vikwazo vinavyowazuia kujikinga wenyewe wamejumuishwa miongoni mwa wafungwa wanaochiliwa mapema.[39] Hali kadhalika, nchini **Ajentina** Mahakama Kuu na ile ya Rufaa ya Jinai zimewajumuisha watu wenye ulemavu miongoni mwa wafungwa watakaoachiliwa.[40] Nchini **Brazil**, Baraza la Haki la Kitaifa, limetoa pendekezo la kukagua, kutathmini upya na kuwaachilia huru wafungwa wenye ulemavu, wakiwemo watoto.[41]

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- **Kupunguza idadi ya wafungwa kwa kuwaachilia walio hatarini, wakiwemo wenye, kuwaachilia wafungwa mapema, kuwaruhusu watumikie kifungo wakiwa nje au kupunguza muda wa kifungo na kupunguza muda wa kukaa rumande** na kuhakikisha wanapokea usaidizi katika jamii kupitia familia na/au huduma zisizo rasmi. Pia, huduma za usaidizi zinazotolewa na watoa huduma wa binafsi na umma.
- **Kutekeleza kanuni za kujikinga** kwenye magereza ili kupunguza hatari ya maambukizi ikiwemo kwa kuwatambua wafungwa wenye ulemavu na kuhakikisha kuwa wanaweza kupata usaidizi, chakula, maji na wanazingatia usafi; walioambukizwa watengwe na wafungwa wasikaribiane. Vifaa vya kujikinga pia vitumike na usafi udumishwe.

**Nyenzo**

- Shirika la Afya Ulimwenguni, Kuzuia na kudhibiti msambao wa COVID-19 katika magereza na sehemu zingine ambako watu huzuiliwa
- Kamati ya Kudumu ya Asasi Mbalimbali ya Umoja wa Mataifa, COVID-19: kuangazia ukiukaji wa haki za kibinadamu

## b. WATUWENYE ULEMAVU WASIO NA MAKAOYANAYOFAA

Watu wenye ulemavu hasa wenye matatizo ya kiakili na walio punguani pia ni wengi miongoni mwa watu maskini zaidi. Watu walemavu wasio na makao na wanaoishi katika makaazi ya dharura na kwenye mitaa ya mabanda wako katika hatari ya kuambukizwa COVID-19 kutokana na msongamano wa watu, ukosefu wa maji, kuishi katika mazingira chafu na kutokana na kuugua magonjwa mengine.

Janga la COVID-19 limesababisha watu wasio na makao, wakiwemo wenye ulemavu, kutafuta usaidizi na makao mengine. Hili limepelekea watu kufurika katika makaazi ya dharura hivyo kusababisha kusambaa kwa virusi. Watu ambao hawawezi kutangamana kwa umbali kutokana na hali ya maisha yao pia wako katika hatari ya kuambukizwa.

**Je, baadhi ya mipango mwafaka ni ipi?**

- Nchini **Marekani**, suala la ukosefu wa makao limeshughulikiwa kupitia mwongozo mahsusi unaowajumuisha watu wenye ulemavu.
- Nchini **Chile,** serikali imetangaza jitihada zaidi katika kutoa huduma za afya kwa wasio na makao.

- Nchini **Ajentina,** zaidi ya vitanda 1,000 viliwekwa katika jengo kubwa litakalotumika kama makaazi ya dharura ili kuwawezesha watu kutokaribiana bila ya kuwawekea masharti mengi ya kiafya.

**Je, ni hatua zipi muhimu ambazo Nchi na washikadau wengine wanaweza kuchukua?**

- **Kuhakikisha kuwa watu walemavu wasio na makao wanaheshimiwa**, na kuwa wanaowapokea wasio na makao wapokee **mafunzo na mwongozo** kuhusu mawasiliano ili kujiepusha na mtafaruku.
- **Kuepuka kuwafurusha watu wanaoishi katika mitaa ya mabanda**, kwani hili linaweza kusababisha ongezeko la msambao wa virusi. Kuwatibu wasio na makao na watu wenye ulemavu wanakoishi na kuwapa makao salama ikiwa yapo.
- **Kutafuta makaazi kadhaa yanayohakikisha watu hawakaribiani**, ikiwemo nyumba za kukodisha, hoteli, vituo vya mikutano na viwanja vya michezo, ambapo usafi umedumishwa na pawe panastahiki.
- **Kutoa huduma za usafi wa umma**, ikiwemo maji, sabuni, mifereji na raslimali zingine ili kuhakikisha maji na vyoo vinapatikana.

**Nyenzo**

- Ripoti ya Mtaalam Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki ya kuwa na makao yanayofaa, Mwongozo kuhusu COVID-19: Kuwalinda wasio na makao
- Ripoti ya Mtaalam Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki ya kuwa na makao yanayofaa, Mwongozo kuhusu COVID-19: Kuwalinda wanaoishi katika mitaa ya mabanda

## NYENZO – ZA JUMLA

- Kamati ya CRPD na Ubalozi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Ufikivu kwa Walemavu, Taarifa Rasmi: Jinsi COVID-19 imewaathiri Watu wenye Ulemavu
- Muungano wa Kimataifa wa Walemavu, Jinsi COVID-19 imeathiri watu walemavu katika kutoka sehemu moja hadi nyingine
- Shirika la Kimataifa la Walemavu na Maendeleo: Hifadhi ya nyenzo kuhusu kujumuishwa kwa walemavu katika kukabilina na COVID-19
- ILO, Hakuna atakayeachwa nyuma, wakati huu, wala kamwe: Kujumuishwa kwa watu wenye ulemavu katika kukabiliana na COVID-19
- Mashirika ya kieneo na kimataifa ya watu wenye ulemavu wa kiakili, Taarifa kuhusu jinsi COVID19 imeathiri watu wenye ulemavu wa kiakili, pamoja na mapendekezo
- Shirika la Umoja wa Maitaifa linajitahidi kuhakikisha kuwa makundi yaliyo hatarini yamejumuishwa katika kukabiliana na COVID-19
- UN ESCAP: Kuhakikisha Watu wenye Ulemavu Wamejumuisha na Haki Zao Kulindwa katika Kukabiliana na Covid-19
- Kamati ya Kudumu ya Asasi Mbalimbali ya Umoja wa Mataifa, COVID-19: kuangazia ukiukaji wa haki za kibinadamu
- UNPRPD, ILO na mashirika mengine, Ulinzi wa kijamii kwa walemavu wakati wa janga la COVID-19
- Ripoti ya Wataalam Maalum wa Umoja wa Mataifa na wataalam huru, COVID-19 inaathiri watu wote: "Kila mtu ana haki ya kuishi"
- Ripoti ya Mtaalam Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu, COVID-19: Je, ni nani anayewalinda watu wenye ulemavu?
- UNFPA, Mwongozo kuhusu Utoaji wa Huduma kwa Njia Inayolinda Haki na Kuzingatia Jinsia katika Kushughulikia Dhuluma za Kijinsia na Kulindwa kwa Haki za Kijinsia na Uzazi kwa Wanawake na Vijana wenye Ulemavu
- UNICEF, Kukabiliana na COVID-19: Kuwashughulikia Watoto na Watu Wazima wenye Ulemavu
- Shirika la Afya Ulimwenguni, Kuwashughulikia watu wenye ulemavu wakati wa janga la COVID-19

- [Shirika la Afya Ulimwenguni, mwongozo wa Kuzuia na Kudhibiti Maambukizi kwa Vituo vya Matibabu ya Muda Mrefu wakati wa janga la COVID-19, Mwongozo wa muda, 21 Machi 2020]
- [Shirika la Afya Ulimwenguni, Kuzuia na kudhibiti msambao wa COVID-19 katika magereza na sehemu zingine ambako watu huzuiliwa]

---

[1] Angalia http://www.sanita.sm/on-line/home/bioetica/comitato-sammarinese-di-bioetica/documents-in-english/documento2116023.html.

[2] Angalia https://www.hhs.gov/sites/default/files/ocr-bulletin-3-28-20.pdf

[3] Angalia https://www.khaleejtimes.com/coronavirus-pandemic/combating-coronavirus-uae-launches-home-testing-programme-for-people-of-determination

[4] Angalia https://www.facebook.com/pg/chrgovph/photos/?tab=album&album_id=2681151298668065&__tn__=-UC-R

[5] Angalia https://www.canada.ca/en/employment-social-development/news/2020/04/backgrounder--covid-19-disability-advisory-group.html

[6] Adelina Comas-Herrera na Joseba Zalakain, “Vifo vinavyohusishwa na msambao wa COVID-19 katika makao ya utunzaji: ithibati ya kimataifa ya mapema ”, International Long term care policy network, 12 Aprili 2020, ukurasa wa 5

[7] Angalia http://www.health.gov.on.ca/en/pro/programs/publichealth/coronavirus/docs/2019_testing_guidance.pdf

[8] Taarifa kutoka kwa mashirika ya kieneo na kimataifa ya watu walemavu pamoja na mapendekezo kuhusiana na janga la COVID-19, inapatikana kwenyehttps://dkmedia.s3.amazonaws.com/AA/AG/chrusp-biz/downloads/357738/COVID19-and-persons-with-psychosocial-disabilities-final_version.pdf

[9] Janga lilipozuka nchini Uchina, kijana wa miaka 16 aliyekuwa akiugua ugonjwa wa kupooza akili aliaga kwa sababu familia yake ilitengwa hivyo wakaishia kumwacha peke yake bila usaidizi

[10] Shirika la Walemavu la Paragwai (SENADIS) lilizindua utumiaji wake wa mitandao ya kijamii ili kutoa maelezo kwa lugha ya ishara, hivyo kuwasaidia wenye matatizo ya kusikia waweze kupata maelezo

[11] Angalia SENADIS, Panamá toma medidas para la inclusión de las personas con discapacidad frente al covid-19, 3.1.

[12] Angalia https://www.health.govt.nz/our-work/diseases-and-conditions/covid-19-novel-coronavirus/covid-19-novel-coronavirus-resources/covid-19-novel-coronavirus-new-zealand-sign-language

[13] Angalia https://coronavirus.gob.mx

[14] Ajentina, Sheria 297/2020, Kipengee cha 6.5.

[15] Mikakati hii inatumika na Nchi, kama vile Kolombia (angalia https://www.minsalud.gov.co/sites/rid/Lists/BibliotecaDigital/RIDE/DE/PS/asif13-personas-con-discapacidad.covid-19.pdf)

[16] Angalia SENADIS, *Panamá toma medidas para la inclusión de las personas con discapacidad frente al covid-19*, 3.3.

[17] Angalia Muungano wa Uingereza na Ayalandi Kaskazini, Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Kuzuka kwa Virusi vya Korona: unachopaswa kufanya na kutofanya, sehemu ya 15

[18] Angalia Secrétariat d’Etat auprès du Premier Ministre chargé des personnes handicapées, kwenye https://handicap.gouv.fr/autisme-et-troubles-du-neuro-developpement/infos-speciales-coronavirus/article/information-covid-19-et-confinement

[19] Angalia OECD, Ugonjwa, *Jinsi Ulemavu Unavyoathiri Ajira. Kuvunja mipaka*, ukurasa wa 23, unaonyesha kuwa utendakazi wa watu wenye ulemavu uko chini ikilinganishwa na wengine: 49% hadi 20%, mtawalia

[20] Angalia, UNDESA, *Ripoti kuhusu Jinsi Ulemavu Unavyohusiana na Maendeleo*, ukurasa wa 157, Mchoro wa II.81**,** unaonyesha kuwa watu wenye ulemavu ni zaidi kwa asilimia 9 miongoni mwa waliojiajiri (Data ya nchi 19)

[21] Bulgaria, Gazeti la Serikali, tarehe 24 Machi 2020, Kipengee cha 12; Shirika la IMF, Sera za kukabiliana na COVID-19, https://www.imf.org/en/Topics/imf-and-covid19/Policy-Responses-to-COVID-19#T

[22] Angalia https://www.argentina.gob.ar/noticias/bono-extraordinario-para-las-personas-con-discapacidad-que-cobran-pensiones-no

[23] Angalia https://informations.handicap.fr/a-prime-solidaire-aah-covid-12818.php

[24] Shirika la IMF, Sera za kukabiliana na COVID-19, https://www.imf.org/en/Topics/imf-and-covid19/Policy-Responses-to-COVID-19#T

[25] Angalia https://www.benefits.gov/benefit/945

[26] K.m. kwa shule za msingi, idadi ya wanafunzi wenye ulemavu wanaokamilisha masomo ni asilimia 56 ikilinganishwa na asilimia 73 kwa wanafunzi wengine

[27] UNESCO inakadiria kuwa kusitishwa kwa masomo kumeathiri zaidi ya asimilia 91 ya wanafunzi wote kote ulimwenguni. Angalia https://en.unesco.org/covid19/educationresponse

[28] Soma kuhusu Idara ya Elimu ya Marekani, Maswali na majibu kuhusu kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu wakati wa janga la virusi vya korona 2019, Machi 2020

[29] Soma https://educacion.gob.ec/wp-content/uploads/downloads/2020/03/Anexo-2-RECOMENDACIONES-A-LOS-DOCENTES-PARA-BRINDAR-APOYO-PEDAGÓGICO-A-LOS-ESTUDIANTES-EN-AISLAMIENTO-EN-FUNCIÓN-DE-PREVENIR-POSIBLES-CONTAGIOS-POR-ENFERMEDADES-RESPIRATORIAS.pdf

[30] Soma kuhusu Uingereza, https://www.gov.uk/guidance/supporting-your-childrens-education-during-coronavirus-covid-19. Pia angalia, https://www.gov.uk/guidance/help-children-with-send-continue-their-education-during-coronavirus-covid-19

[31] Shirika la Afya Ulimwenguni, *Jinsi COVID-19 imechangia katika dhuluma dhidi ya wanawake Hatua ambazo sekta ya afya inaweza kuchukua*, kwenye https://apps.who.int/iris/bitstream/handle/10665/331699/WHO-SRH-20.04-eng.pdf

[32] UNDESA, Disability and Development Report, pp. 7, 16, 113-115, 249-252, at https://social.un.org/publications/UN-Flagship-Report-Disability-Final.pdf; Ripoti ya Mtaalam Maalum kuhusu haki za watu wenye ulemavu, A/72/133, aya ya 35

[33] Emma Pearce, *Kuwajumuisha Watu wenye Ulemavu katika Mpango wa GBV wakati wa Janga la COVID-19*, kwenye https://gbvaor.net/sites/default/files/2020-03/Disability%20Considerations%20in%20GBV%20programming%20during%20COVID_Helpdesk.pdf

[34] Peru, Ministerio de Desarrollo e Inclusión Social, *Resolución Viceministerial N° 001-2020-MIDIS/VMPES*, 24 Aprili 2020, kwenye https://www.gob.pe/institucion/midis/normas-legales/484313-001-2020-midis-vmpes

[35] Huduma za Kitaifa za utoaji ushauri nasaha kwa waliopitia dhuluma za kimapenzi, vurugu za kifamilia na kinyumbani, nchini Austrelia https://www.1800respect.org.au/accessibility/ ; Msambao wa virusi vya Korona nchini Uingereza (COVID-19): usaidizi kwa wahasiriwa wa dhuluma za kinyumbani https://www.gov.uk/government/publications/coronavirus-covid-19-and-domestic-abuse/coronavirus-covid-19-support-for-victims-of-domestic-abuse#disability-specialist-services

[36] Shirika la Penal Reform International, Hali Ilivyo kwenye Magereza Kote Ulimwenguni 2020, kwenye https://cdn.penalreform.org/wp-content/uploads/2020/04/Global-Prison-Trends-2020-Penal-Reform-International.pdf

[37] Mwongozo: Jinsi virusi vya Korona (COVID-19) vimeathiri magereza, kwenye https://www.gov.uk/guidance/coronavirus-covid-19-and-prisons

[38] https://www.prisonpolicy.org/virus/virusresponse.html

[39] Kolombia, Decreto legislativo 546, 14 Aprili 2020, kwenye https://dapre.presidencia.gov.co/normativa/normativa/DECRETO%20546%20DEL%2014%20DE%20ABRIL%20DE%202020.pdf

[40] Ajentina, Mahakama Kuu ya Kitaifa, *Acordada 10/2020*, na sheria ambatani, Mahakama ya Rufaa ya Jinai, *Acordada 9/2020*, kwenye https://cnpt.gob.ar/wp-content/uploads/2020/04/Acordada-9.20-CFCP.pdf

[41] Brazili, Baraza la Haki la Kitaifa, pendekezo la 62, 17 Machi 2020, kwenye https://www.cnj.jus.br/wp-content/uploads/2020/03/62-Recomenda%C3%A7%C3%A3o.pdf